

MTAALA MPYA WA UMILISI
GREDI 4 - MWAKA 2020
KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa moja dakika 40

Jina _____ TAREHE: _____

Jinsia:

Mume

Mke

Jina la kaunti _____ kaunti ndogo _____

Jina la shule _____

VIWANGO VYA KUTATHMINI

	Kuzidisha matarajio	Kufika matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
SEHEMU (1) Kusikiliza na kuongea	Alama (4) 13 - 15	Alama (3) 10 - 12	Alama (2) 5 - 9	Alama (1) 0 - 4
SEHEMU (2) Kusoma	9 - 10	6 - 8	4 - 7	0 - 3
SEHEMU (3) Sarufi	13 - 15	10 - 12	5 - 9	0 - 4
SEHEMU (4) Jumla	35 - 40	26 - 32	14 - 25	0 - 11
Mwalimu				

Maagizo

1. Jibu maswali yote kwa kiswahili.
2. Tathmini hii ina sehemu tatu **kusikiliza na kuzungumza, kusoma na sarufi.**
3. Jibu maswali yote kulingana na maagizo uliyopewa.

SEHEMU YA KWANZA

KUSIKILIZA NA KUONGEA (Alama 15)

1. (a) **Andika maneno ambayo mwalimu atakusomea.**

Sikiliza kwa makini, kisha uandike

(Alama 5)

- (i) _____
- (ii) _____
- (iii) _____
- (iv) _____
- (v) _____
- (vi) _____

- (b) **Tegua vitendawili hivi**

(Alama 2)

- (i) Teketeke huzaa gumugumu na gumugumu huzaa teketeke

(yai, macho, nyayo)

- (ii) Huwa safi kikiwa cheusi na kichafu kikiwa cheupe

(kalamu na kitabu, ubao)

- (c) **Taja wakati wa maamkuzi na maagano haya.**

(Alama 3)

(asubuhi, jioni, aduhuri, wakati wowote, usiku)

- (i) Hujambo _____
- (ii) Lala unono _____
- (iii) Sabalkheri _____

- (d) **Kamilisha methali hizi.**

(Alama 2)

- (i) Pole ole ndio _____
- (ii) Mtoto wa nyoka _____

- (e) **Ambatanisha maneno haya ya upole ipasaavyo. Fuata mfano.**

Zaa	makalio
kuendesha	mjamzito
matako	kujifungua
kuwa na mimba	kuhara

SEHEMU YA PILI

SARUFI (Alama 20)

2(a) Soma kifungu hiki kisha uchagua nomino kutoka kifungu. (Alama 5)

Mwalimu wangu anapenda kufunza lugha ya Kiswahili. James husoma vizuri katika kipindi cha lugha. Jumatatu masomo ya asubuhi, Naomi pia husoma ufahamu kwa ufasaha, kweli watu wa Mombasa hupedna kiswahili kuliko wengine.

- (i) _____
- (ii) _____
- (iii) _____
- (iv) _____
- (v) _____

(b) Tafuta vitendo kumi katika mraba huu. (Alama 10)

Mfano pika

s	h	u	p	a	k	u	a
u	a	b	a	n	c	p	c
g	s	f	k	o	k	i	p
u	h	k	i	h	r	k	a
a	o	i	p	s	s	a	n
m	n	a	m	s	h	a	g
t	a	n	d	i	k	a	a
e	p	f	a	g	i	a	n
l	o	s	a	n	i	k	a

Vitendo

- (i) _____
- (ii) _____
- (iii) _____
- (iv) _____
- (v) _____
- (vi) _____
- (vii) _____
- (viii) _____
- (ix) _____
- (x) _____

(c) Andika sentensi hizi upya. Tumia viwakilishi.

(sisi, wewe, yeye, wao) badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.

(Alama 2)

(i) Damiana analima shamba

(ii) Wanafunzi tutafunga lini?

(d) Pigia mstari viunganishi katika sentensi hizi.

(Alama 2)

(i) Maembe, machungwa na mananasi ni matunda.

(ii) Nilimshauri ila hakisikia.

(e) Maneno polepole, vizuri, haraka haraka, upesi na darasani ni

(Alama 1)

(nomino, vielezi, viwakilishi, viunganishi)

SEHEMU YA TATU

KUSOMA (Alama 10)

Soma kifungu kisha ujibu maswali.

Asubuhi moja, mama alikuwa tayari kuondoka akielekea kazi pale, Tembea Tuonane. Aliwaita watoto wake na kuwaambia wamsikilize kwa makini.

“Ninaenda kazini. Nimeacha kila kitu kikiwa sawa hapa nyumbani. Ninajua mnapenda mchezo. Nikirudi nipate nyumba na vyombo vyote vichafu. Nipate pia mmekula chakula chote hata cha mtoto, sawa?” mama aliwambia, kwa kujua mazoea ya watoto wake. “Sawa, mama!” wote walijibu. Mama aliondoka akaenda kazini.

Maswali.

(i) Nani alikuwa anaenda kazi asubuhi ile? _____

(ii) Mama aliwataka watoto wasikilize kwa _____

(iii) Mama anaposema, nikirudi nipate nyumba na vyombo vyote ni vichafu ana maanisha nini? _____

(iv) Watoto wale walikuwa na mazoea yapi? _____

(v) Je, unafikiri mama aliporudi jioni alipata watoto wamefanya nini? _____